TAARIFA YA MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE

1. UTANGULIZI

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ni taasisi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyoanzishwa kwa sheria namba 8 ya mwaka 2011 kutoka Idara ya Anga kama ilivyokuwa inatambulika awali na kuanza kazi zake rasmi mwezi Agosti mwaka 2011.

2. MUUNDO WA MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege iko chini ya Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji ambapo inaongozwa na Bodi ya Wakurugenzi yenye wajumbe 7, Kiutendaji Mamlaka inaendeshwa na Mkurugenzi Mkuu akiwa na Idara tano (5) na vitengo 6, ambazo ni:-

1. Idara ya Viwanja
2. Idara ya Fedha na Utawala
3. Idara ya Ufundi
4. Idara ya Biashara na Masoko
5. Idara ya Mipango na Miradi.

Aidha Mamlaka ina vitengo 6 vinavyojitegemea ambavyo ni:-

1. Kitengo cha Sheria
2. Kitengo cha Ukaguzi wa Hesabu wa Ndani.
3. Kitengo cha Viwango (Compliance)
4. Kitengo cha Manunuzi
5. Kitengo cha Uhusiano
6. Kitengo cha IT

Viwanja vya Ndege vinavyoendeshwa na Mamlaka.

- Kiwanja cha Kimataifa cha Abeid Aman Karume cha Unguja
- Kiwanja cha Ndege cha Pemba,
- Kiwanja cha Ndege cha Kigunda

Aidha, Katika kutanua na kuimarisha huduma za usafiri wa anga Zanzibar, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar inaendelea na taratibu za kujenga viwanja vya vyengine vya Ndege katika maeneo ya Domokuchu (Paje), Mwambe Mkoani Pemba na Kigomasha kaskazini Pemba.

3. MAJUKUMU YA MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE

Majukumu ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar yameelezwa kwa ukamilifu na sheria namba 8 ya mwaka 2011, kifungu namba 5, ambapo miongoni mwa majukumu makuu yaliyotajwa ni:-

- Kuviendesha na kuvisimamia viwanja vya ndege vya Serikali katika Zanzibar pamoja na kuishauri Serikali katika uendeshaji wa Viwanja vya Ndege.
- Kusimamia usalama kwa safari za abiria na mizigo katika viwanja vya ndege vya Serikali.
- Kutekeleza taratibu na sheria zote za uendeshaji wa viwanja kama zinavyoelekezwa na Tanzania Civil Aviation Authority (TCAA) na International Civil Aviation Organisation (ICAO).

HALI YA RASILIMALI WATU

Katika kutekeleza majukumu hayo makuu Mamlaka kwa hivi sasa ina jumla ya wafanyakazi 736 wakiwemo wanaweke 326 na wanaume 410, ambao wametokana na kada tofauti za kielimu zikiwemo ufundi, mipango, utawala, uhasibu, Ukaguzi, IT, Aviation, sheria n.k

Kada ya usafiri wa anga inakwenda sambamba na kada nyengine za elimu ziliyopo na ndio maana mara nyingi mafunzo ya kada hii huwa ni maalum na ni ya muda mfupi. Kutokana na uhalisia wa kada hii, karibu Nyanja zote za taaluma ni muhimu na huhitajika katika 'Proffesion' ya usafiri wa anga

4. SHERIA NA TARATIBU ZINAZOONGOZA VIWANJA VYA NDEGE

Ukiwacha sheria namba 8 ya Mamlaka ya Viwanja vya ndege (The Zanzibar Airports Authority Act, No. 8 of 2011), pamoja na Sheria namba 9 ya Viwanja vya Ndege (The Zanzibar Aerodromes Act, No. 9 of 2011), Mamlaka vile vile inaongozwa na sheria ya utumishi wa umma, sheria namba 2 ya 2011 na kanuni zake za 2014 katika kuendeleza na kuwaongoza watendaji wake Aidha Mamlaka inatumia na sheria mama nyengine zilizowekwa na Serikali kama vile sheria za fedha, manunuzi, mazingira n.k

5. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA HATUA ZA AWALI ZA MUAJIRIWA

- Kanuni namba 9: Mtumishi yeyote ambae ameajiriwa kwa mara ya kwanza atalazimika kuwemo katika majaribio ya utumishi kwa muda wa miezi kumi na mbili kuanzia tarehe ya kuajiriwa.

- Mtumishi wa umma aliye katika muda wa majaribio atakuwa na haki na fursa zifuatazo:- (a) Kulipwa mshahara na posho anazostahiki kwa mujibu wa kazi yake; (b) Kumkumbusha muajiri wake ili amthibitishe baada ya kumaliza muda wa majaribio; (c) Kuomba likizo la kawaida la mwaka.

- Mtumishi wa umma aliyekuwepo katika muda wa majaribio hatoruhusika kwenda katika mafunzo ya muda mrefu mpaka baada ya kutimiza miaka miwili ya ajira yake.

Utaratibu wa kazi ndani ya Mamlaka

- Wafanyakazi wa utawala wanafanyakazi kwa utaratibu wa masaa 8 kwa siku ndani ya siku 5 kwa wiki na hupumzika siku ya Jumamosi na Jumapili au siku ya mapumziko ya kitaifa.

- Wafanyakazi wa Uendeshaji wanaingia kazini kwa shift ndani ya masaa 24 kwa siku saba. Cha kuzingatia masaa ya mtumishi hayatozidi masaa ya kawaida yanayokubalika kisheria kwa wiki na mwezi.

- Mfanyakazi wa Mamlaka anaweza kupangiwa kazi sehemu yoyote kilipo kiwanja cha ndege ndani ya Zanzibar.

Utaratibu wa hatua za kinidhamu

- Mamlaka inatumia Sheria ya Utumishi wa Umma na kanuni zake katika kuchukua na kutekeleza hatua za kinidhamu, ambapo hatua hizo hutekelezwa na Menejimenti pamoja na Bodi kupitia utaratibu uliwekwa kisheria.

- Suala la kufuata maadili, uadilifu na uaminifu ni muhimu sana katika viwanja vya ndege

Utaratibu wa kufanya kazi kati ya wafanyakazi wa viwango tofauti vya elimu.

- Mamlaka inafanya ajira hii kwa kuchukuwa vijana wenye sifa mbali mbali za kielimu ambapo baada ya kukamilika uajiri huu waajiriwa wote watapatiwa mafunzo maalumu yanayohusiana na kazi zao, mafunzo

ambayo yatachukuwa wastani wa miezi miwili na watakaofaulu watapatiwa leseni ya kufanyia kazi husika.

- Baada ya kukamilika mafunzo hayo wafanyakazi wataendelea kuwa katika muda wa majaribio kuangalia uwezo wao katika kazi kwa kuzingatia sheria na kanuni za utumishi.
- Waajiriwa wote waliopo katika kipindi cha majaribio watafanyiwa uhakiki (appraisal) baada ya kukamilika muda wao wa majaribio na wale waliokidhi viwango hitajika watathibitishwa na watapangiwa nafasi zao kwa mujibu wa sifa zao ambapo wale wenye Degree watapangiwa kama maofisa (suppervisors), wenye Diploma watapangiwa kama maofisa wasaidizi na wenye Form VI watakuwa wasaidizi maofisa.
- Wafanyakazi walioajiriwa na ngazi ya Diploma hawatohisabiwa kuwa na kiwango cha shahada ya juu (Degree) chini ya miaka 2 tangu alipoajiriwa.
- Wafanyakazi walioajiriwa na ngazi ya Form VI hawatohisabiwa kuwa na kiwango cha shahada ya juu (Degree) chini ya miaka 3 tangu alipoajiriwa.